SAGCOT
SOUTHERN AGRICULTURAL GROWTH CORRIDOR OF TANZANIA



# Ubia Mkakati wa Kuku

## Muhtasari

Sekta ndogo ya ndege wanaofugwa nchini Tanzania inaundwa na mifumo ya uzalishaji wa kienyeji na kibiashara. Ndege wanaofugwa nchini wengi ni kuku asilimia (90%) na kiasi kidogo kilichobaki ni bata, mbuni, njiwa na kanga. Kwa mujibu wa Chama cha Wazalishaji wa Ndege wanaofugwa Tanzania (TPBA), kuku wa kienyeji wameonyesha kuwa ni chanzo kikubwa cha usalama wa chakula, kipato cha kaya kwa watu waishio vijijini, hususan makundi yaliyosahaulika kama wanawake na watoto.
Ufugaji kibiashara wa kuku bado ni wa kiwango cha chini kutokana na ukosefu wa ujuzi na utaalam wa jinsi ya kufuga, ukosefu wa mitaji ya uwekezaji, masoko yasiyokuwa na utaratibu unaofaa wa kuku na mazao yao, uzalishaji usiokuwa na uhakika wa vifaranga wenye umri wa siku moja, ukosefu wa uzalishaji wa chakula bora cha kuku, gharama kubwa za utabibu mifugo, gharama kubwa za chakula na ukosefu wa viwanda vinavyochakata kuku na mazao yatokanayo na kuku. Ulaji wa nyama ya kuku kwa kila mtanzania inakadiriwa kuwa ni kilogramu 15 kwa mwaka (FAO 2015). Kupitia Ubia Mkakati wa Mnyororo wa Kuku, SAGCOT inafanya kazi kwa karibu na wabia kushughulikia changamoto na fursa zilizopo kwenye sekta hii ndogo.

## Wadau Muhimu walioko kwenye Ubia wa Kukui

- Sekta ya Umma
- Sekta Binafsi
- Washirika wa Maendeleo
- Asasi za Wakulima
- Wakulima mmoja mmoja
- Asasi za Kiraia



## Mpango wa Kukuza Kilimo Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (SAGCOT)

Mpango wa SAGCOT ni ubia kati ya sekta ya umma na binafsi unaolenga kuchochea Uwekezaji kwenye Kilimo biashara katika ukanda wa kusini mwa Tanzania. Kituo cha SAGCOT kinafanya kazi kama dalali wa ubia na kitovu cha habari kwa wabia wa SAGCOT katika kuwezesha uwekezeshaji kwenye minyororo ya thamani inayoshirikisha jamii na kuzingatia uhifadhi endelevu wa mazingira. Kituo cha SAGCOT kinakuza na kuwezesha ubia mkakati ili kuimarisha mbinu shirikishi na kuboresha ushirika uliopo miongoni mwa wadau muhimu ndani na nje ya minyororo ya thamani iliyopewa vipaumbele.

## Mnyororo wa thamani wa kuku una umuhimu gani?

Mnyororo wa thamani wa kuku unawakilisha mojawapo wa harakati zinazotuwezesha kuondoa umaskini kwa njia ya kutoa ajira kwa wanawake na vijana. Mbali ya hayo, mnyororo wa thamani unaendelea kuwa ni nguzo muhimu ya kuchangia katika kuongeza lishe na usalama wa chakula. Mabadiliko yanayoendelea katika tasnia ya kuku , hususan miongoni mwa wafugaji wadogo yanaendelea kuboresha hali ya maisha kwa kuongeza kipato na kuboresha hali ya lishe katika jamii.
Kwa mujibu wa takwimu za FAOSTAT, mwaka 2017, Tanzania ilichakata takriban tani za ujazo 104,000 za nyama ya kuku huku kiwango cha ukuaji wa jumla wa miaka 5 (CAGR) wa asilimia (4%). Zaidi ya hilo, uzalishaji wa nyama na mayai,kuku ni chanzo kikubwa cha mbolea na chanzo muhimu cha mtiririko wa mapato kwa kaya za wafugaji. Kwenye jamii nyingi hapa nchini kuku pia wanatumika kama hazina ya utajiri na vilevile hutumika kama raslimali fedha kwenye malipo baada ya kufanya biashara baina ya mtu na mtu/ jamii moja na nyingine.

## Kubadilisha hali ya usalama wa chakula kwa wakulima na kuboresha hali ya maisha katika kaya

Ongezeko la ufugaji wa kuku husababishwa na ukuwaji wa haraka wa miji kutokana na kukua kwa mahitaji ya soko la kuku maeneo ya mijini na pembezoni mwa miji na vijijini. Nchini Tanzania, asilimia (96%) ya wakulima wafugaji hufuga kuku wa kienyeji, kiasi kidogo cha idadi ya kuku mpaka 20 ambapo huzalisha asilimia (94%) ya nyama na mayai maeneo ya vijijini. Kuna tofauti ya mahitaji ya soko kulingana aina ya kuku na mbegu yake maeneo ya mjini na vijijini. Ulaji wa kuku unategemea watu wenye kipato cha kati na cha juu waishio maeneo ya mijini, lakini mahitaji yapo maeneo yote nchini.

## Kutafuta masuluhisho ya kudumu katika mnyororo wa thamani

Kuku wa kienyeji wanaweza kumfikia mlaji moja kwa moja ambapo kuku wa kisasa mara nyingi hupitia kwa msambazaji/muuzaji wa nyama na mayai, hii inasababisha kiasi kikubwa cha kuku wa kisasa ambao hufugwa na mkulima mfanyabiashara kwa kipindi fulani cha muda ukilinganisha na idadi ndogo ya kuku wa kienyeji ambao hufugwa na wakulima/wafugaji wengi kwenye kaya. Kuku wa kienyeji hufugwa kwenye makundi madogo ambapo mara nyingi huachwa watembee maeneo ya wazi wakitafuta chakula, mfumo huu wa ufugaji hutumia kiasi kidogo cha pembejeo. Kuku wa kienyeji/asili wanaotoa lishe muhimu na ni chanzo cha kipato kwa kaya nyingi ziishizo vijijini wakati kuku wa kisasa hufugwa kwenye makundi makubwa katika mfumo wa kibiashara uliowekewa miundombinu mizuri na nyumba za kufugia.

## Umuhimu wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi

Tathmini ya mnyororo wa thamani wa kuku katika ukanda inaonyesha kuwa ufugaji wa kuku unaendeshwa na sekta binafsi lakini inasimamiwa kisera/kisheria na sekta ya umma hivyo basi inahitaji kuwepo ubia wa sekta binafsi na umma. Ubia mkakati wa Kuku huweka pamoja wadau mbalimbali hususani wabia wa sekta binafsi na ya umma; pia ubia huu ni jukwaa la mashauriano kwa wadau kuweka pamoja maslahi yao na nguvu ya pamoja ya ushawishi katika kuendeleza na kumarisha mnyororo wa thamani wa kuku.

Ubia Mkakati wa Kuku unaundwa na wabia 22 wakiwemo wafugaji wadogo wa kuku, Sekta binafsi kama vile Silverlands, AKM Glitters, Tanfeed (Moragg), NMB, CRDB, Agrovets; sekta ya umma wakiwemo Sekretarieti za Mikoa, OR-TAMISEMI, Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGAs), Kituo cha Uwkezaji Tanzania (TIC), Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Vyuo vya Utafiti wa Mifugo (TALIRI), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Asasi za Wanachama wa Sekta ya Kuku kama vile Tanzania Animal Feed Manufacturer Association(TAFMA), Tanzania Poultry Breeders Association, Poultry Layers Association.

## Kusaidia muunganiko na minyororo mingine ya thamani

Kutokana na mahitaji makubwa ya chakula cha kuku katika ufugaji wa kibiashara wa kuku, sekta hii ndogo imeweza kusaidia muunganiko kwa minyororo mingine ya thamani ambayo huzalisha bidhaa au huduma hususan bidhaa kama mahindi ambayo ni kiambatishi kikubwa kwenye chakula cha kuku kama vile mashudu ya alizeti na soya ambayo ni viambatishi kwenye chakula cha kuku.

## Husaidia kuboresha rutuba ya udongo

Kinyesi cha kuku kinatumika kama mbolea hai ambayo huongezea udongo virutubisho kwa ajili ya uzalishaji wa Kilimo cha mbogamboga na matunda, kwenye Mashamba madogo yaliyoko kwenye makazi katika kaya. Kinyesi cha kuku kina kiasi cha kutosha cha Nitrogen, Phosphorus, na Potassium ambavyo ni mojawapo ya viasili muhimu katika kurutubisha udongo wenye kiasi kidogo cha hewa ya Nitrojeni. Kiasi kikubwa cha mboleo kinapatikana kutoka kwenye mbegu bora ya kuku (wa nyama, wa mayai, aina ya Kuroiler and Sasso), ambao kawaida hufugwa na kuangaliwa wakiwa wamefungiwa ndani katika nyumba au mabanda.


### Kwa taarifa zaidi wasiliana nasi kupitia:

SAGCOT Centre Limited

Gholofa ya 5, Jengo la Ikon
Barabara ya Bains, Masaki
S.L.P 80945
Dar es Salaam, Tanzania

**Simu:** +255 22 260 1024
+255 22 260 0146
**Faxi:** +255 22 260 2368

**Barua Pepe:** info@sagcot.co.tz
**Tovuti:** www.sagcot.co.tz


## Matokeo jumuishi na endelevu.

**Umilikaji na mgawanyo wa faida:** Tofauti na ng'ombe, kondoo na mbuzi, ufugaji mdogo wa kuku ni chanzo cha ajira kwa makundi tofauti ya watu kwenye jamii zetu. Wafugaji wa kuku walio wengi ni wanawake na kwa kiasi kikubwa faida za kifedha wanazopata kutokana na mauzo ya kuku walio hai na mayai hutumiwa na wanawake. Vijana wanajihusisha na ununuzi na uuzaji wa mayai na kuku walio hai na baadhi yao wakijushughulisha na biashara za kuongeza thamani kama vile kukaanga kuku na mayai. Yatima na walemavu wa viungo vya mwili wamejiunga katika vikundi vya ujasiriamali ambavyo huzalisha mayai na nyama kupitia miradi iliyopo kwenye kongani kama vile mradi wa Africa Bridge. Wafugaji wengi wa kuku kibiashara huajiri wafanyakazi/vibarua hususani wanaume na wanawake kwa wastani wamfanyakazi/kibarua mmoja kwa kila mfugaji mmoja wa kuku kibiashara.

**Kusaidia uwekezaji kwa wafugaji wadogo:** Kama mkakati wa biashara, wafugaji na wachakataji wa kati na wakubwa wanajenga uwezo kwenye jamii kupitia uwekezaji wa jumla unaobadilishana thamani na kuwapatia huduma za ugani. Msaada pia hutolewa kwenye vikundi vya wafugaji wadogo ili kutengeneza soko la moja kwa moja la uhakika; vilevile kutoa msaada wa kitaalamu kwa wafugaji wadogo kuimarisha ubora wa bidhaa wanazozalisha kwenye mnyororo wa thamani, Makampuni ya Silverlands na AKM Glitters ndio wazalishaji wakubwa wa vifaranga wenye umri wa siku moja na chakula cha kuku, wakishirikiana na wabia kama vile chuo cha Utafiti wa Mifugo (TALIRI) na Chuo cha Kimataifa cha Utafiti wa Mifugo (ILRI) ambao wametoa msaada kwenye mradi wa African Chicken Genetic Gain unaolenga kuongeza uzalishaji wa mbegu bora ya kuku aina ya Kuroiler na Sasso.

## Changamoto muhimu

- **Uzalishaji wa mbegu bora ya vifaranga vya kuku wenye umri wa siku moja na kuku-** Uzalishaji mdogo na usambazaji wa vifaranga wenye umri wa siku moja, na mfumo usiotosheleza wa kutafiti magonjwa, upungufu wa kutoa chanjo na matibabu kwa kuzingatia muda muafaka, matumizi madogo ya teknolojia ya uanguaji mayai na uzalishaji wa chakula cha kuku.
- **Kuongezeka thamani kwa kuku na bidhaa zitokanazo na kuku-** Ukosefu wa machinjio mazuri ya kuku ili kuhakikisha nyama salama inafika sokoni, kukatika kwa umeme mara kwa mara, masuala yahusuyo udhibiti ubora na ukosefu wa uelewa na maarifa juu ya uchakataji na ufungashaji wa kuku wa kienyeji.
- **Upatikanaji wa huduma za kifedha kwa watendaji katika mnyororo wa thamani wa kuku-**Kukosekana kwa utamaduni wa kutafuta fedha binafsi ya kuwekeza kwenye mnyororo wa kuku, na uwezo mdogo wa kusaidia makundi ya wanawake na vijana kutafuta fedha kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuajili ya kuwekeza katika biashara ya kuku.
- **Mifumo ya soko isiyo na muundo mzuri –** soko lisilotabirika na kukosa muundo mzuri kwa sekta ndogo ya kuku, wafugaji wachache wa kuku ambao wanatumia Huduma za Maendeleo ya Biashara, uelewa mdogo wa jamii kuzingatia ulaji wa bidhaa bora zitokanazo na kuku kama chanzo cha lishe na uelewa mdogo wa wateja kuhusu upatikanaji wa vifaranga wa kuku wenye umri wa siku moja.
- **Sera na mazingira wezeshi ya biashara-** Hakuna maabara kwenye ngazi ya kanda zinazopima ubora wa chakula cha kuku, usimamizi na ufuatiliaji duni kuhusu orodha ya wauzaji wa chakula cha kuku viambatishi vinavyotolewa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ukosefu wa wakaguzi wa chakula katika ngazi ya Mamlaka ya Serikali za mitaa kuhakikisha kunakuwepo na uwekaji viwango vya kisera katika ngazi ya taifa.